


# Mipango ya miradi katika udugu

Mwongozo juu ya Miradi ya UEM



# *Yaliyomo*

Dibaji .....	3
Utangulizi .....	4
I. Nafasi ya (Wajibu wa) Fedha katika Udugu:	
Mtazamo wa Ki-indonesi .....	5
II. Namna UEM Inavyowezesha Miradi na Mipango Mbalimbali	
ya Maendeleo .....	8
III. Hatua Mahususi za kufikia Mradi kamili: Kuanzia Wazo	
hadi Utekelezaji wake .....	12
IV. Kibali cha UEM kwa Miradi ya Udugu .....	18
V. Mifano Halisi Kutoka Maeneo Mbalimbali .....	20
VI. Vielelezo .....	24
a) Mfano wa Namna ya Kutengeneza au Kuandika Mradi	
b) Maombi ya Kibali cha UEM kwaajili ya Mradi wa Udugu	
Mwandishi, Anwani .....	27

# Dibaji

Waheshimiwa mnaoshiriki katika huduma ya udugu, mabibi na mabwana,

Chapisho hili mnalolisoma, ni mwongozo wa namna ya kupanga miradi ya udugu katika umoja wetu wa UEM. Mwongozo huu ni matokeo ya patano au pendekezo lililotolewa na wajumbe wa Mkutano wa Kimataifa wa Udugu wa makanisa yote wanachama wa UEM uliofanyika mwezi Julai mwaka 2012 katika kitongoji cha Parapat, mjini Sumatra, nchini Indonesia. Kwa lugha ya wenyiji wa mahali ulipofanyikia mkutano huu yaani lugha ya watu wa mto Toba, neno Parapat linamaana ya "Njooni pamoja" au "kusanyikeni pamoja." Ni imani yangu kubwa kwamba chapisho hili litaleta chachu na motisha kwa makundi yote ya udugu ndani ya UEM kuungana kwa pamoja katika kutekeleza miradi mbalimbali, kwa mitazamo tofauti, lakini pia kufahamiana zaidi na zaidi. Kwa upande wetu sisi kama UEM makao makuu, tunapenda kuwatia moyo katika kuweka mwongozo wa pamoja wa namna ya utekelezaji wa miradi kwa pamoja, kama makanisa wanachama wa UEM katika mabara matatu. Kusudi letu ni kuongeza uwazi, usawa, uendelevu, bila upendeleo.

Hii inamaanisha kupanga, kufuatilia na kufanya tathimini ya miradi kunatakiwa kusiwe kwa maneno matupu bali ziwe ni hatua muhimu katika kuhakikisha kuwa miradi yenu inazaar matunda.

Ninapenda kuwatia moyo na kuwaomba muige mfano wa ufanisi wa UEM katika utekelezaji wa miradi yake. UEM kama mtoakibali wa miradi ya udugu iliyokubaliwa, iko tayari kutoa msaada wa ushauri wa karibu kwa miradi mbali mbali kila ushauri unapohitajika. Huenda ni kwa njia hii mtawezza kuona fursa zilizomo ndani ya udugu huu. Ni ubunifu wa namna gani wa miradi unaoweza kutekelezwa Ujerumani, Asia au Afrika? Ni kwa namna gani tunaweza kubuni na kutekeleza miradi kwa pamoja na mhusika wa tatu (mashirika mengine nje ya UEM na makanisa wanachama)? Ifike mahali tuache fikra za njia au namna moja tu yaani UEM, na badala yake tufikirie juu ya UEM kama mtandao (network).

Mtandao huu unauzoefu wa miaka mingi katika kuunganisha na kujadiliana na makundi mbalimbali ya udugu na mtandao huu unayaframamu vizuri makundi haya yote ya udugu. Udugu una-shamiri pale tunaposhauriana, tunapoonyana au tunapojadili changamoto mbalimbali kwa pamoja hususanji juu ya mtazamo wetu wa imani katika Mungu mmoja.




Wenu katika udugu

*Dr Fidon R. Mwombeki  
Katibu Mkuu wa UEM*

# Utahangulizi

4

Miradi inahistoria ndefu au ni utamaduni wa muda mrefu katika udugu ndani ya kanisa. Kutokana na imani iliyojengeka juu ya mafundisho yanayosisitiza juu ya umuhimu wa kugawana utajiri au kumsaidia mhitaaji au kama njia ya kuonyesha mshikamano, miradi mingi katika udugu asili yake ni maeneo yenye uhitaji mkubwa kama vile Afrika na Asia. Shule za chekechea na vituo vya watoto yatima vimejengwa, tasisi za mikopo midogo midogo zimeanzishwa, miradi ya maji na ile ya umeme wa nguvu ya jua (solar) vimeanzishwa. Maranyingi kazi ya miradi katika udugu inakwenda mbali zaidi ya msaada wa vitu. Mfano ni pale ambapo baadhi ya maeneo mradi wa maji unakuwa pia ni fursa ya namna ya kupambanua na kutathimini ni kwa namna gani mtu aweza kutumia maji kwa manufaa. Uwezekano wa ubunifu wa namna ya miradi unajitokeza, na kuititia mwongozo huu, tunakualika uweze kubuni miradi ya udugu kwanjia ya kitaalam zaidi na kujikita au kufuata hatua zote mpya zinazohitajika katika utekeleza miradi katika udugu.



UEM inautajiri wa uzoefu katika utekelezaji wa miradi ya udugu. Katika makundi zaidi ya miamoja ya udugu kati ya makanisa, sharika na taasisi mbali mbali za makanisa, miradi imekuwa mhimili mkubwa wa udugu. Kwa sehemu kubwa, miradi hii ya udugu imesaidia katika kubadilisha hali ya maisha ya watu katika jamii mbalimbali. Miradi yenyeufanisi au miradi bora, inafaida kwa udugu kwa pande zote zinazoshirikiana: inaongeza kuaminiana, inafurahisha, pia inaongeza motisha ya kushirikiana kwa miradi mingine mbeleni. Lakini miradi inapokosa ufanisi katika utekelezaji wake, basi matokeo yake huwa kinyume na hayo chanya yaliyotajwa: udugu unakuwa mashakani, kukatatamaa

na mkaanganyiko vinadhoofisha udugu pamoja na kuharibu mawasiliano na mahusiano kwa ujumla. Mwongozo huu wa sasa, unakusudia kukuwezesha wewe pamoja na kundi lako la udugu kubuni miradi yenyeufanisi na endelevu. Tunategemea kutoa maelezo yatakayoelezea kwa ufasaha njia na hatua za kutengeneza mradi, na kufanya ziwe njia zinazoweza kutumika katika mipango yenu ya udugu (Tazama ukurasa wa 12). Miradi ya udugu haiwezi kuchukua na wala isije ika-chukua nafasi ya kazi za kitaalam za miradi. Badala yake, miradi midogo yote ipangwe kwa umakinini, kuwe na ufuutiliaji pamoja na usimamizi mzuri na ifanyiwe tathmini. Uwazi na uwajibikaji ni mambo ya lazima kwa wanachama wote wa UEM: Mambo haya yanadumisha na kuongeza matumaini katika kufanya kazi za udugu.

Tunawaalika ninyi nyote kuungana katika kupanua wigo wa miradi iliyopo sasa na kukuza na kubuni miradi ya udugu ndani ya UEM. Miradi haitakiwi kutumiwa kama njia ya mmoja kuwa mlezi wa mwingine, bali yote haya yafanyike huku udugu ukizingatia usawa. Tunapenda usawa katika udugu uendelee kuwa kipimo mahususi hata tunapoendelea kuhusiana kwanjia ya kusaidiana kupitia miradi. Usawa katika kupanga, katika ufuutiliaji wa karibu na katika kutathmini miradi ni mambo yanayoweza kuudumisha usawa baina ya makundi ya udugu. Hata katika mfumo huu mpya wa namna ya kupanga na kutekeleza miradi, usawa baina ya makundi ya udugu unaendelea kuonekana. Kwa mfano, kuna makundi ya udugu ambayo yameanzisha miradi mbalimbali ya namna hii. Kwa mfano, mradi unaowaunganisha vijana katika kampeni ya utunzaji wa mazingira, au mradi wa uundwaji wa kundi la muziki linaloshirikisha vijana kutoka makundi mbalimbali ya udugu kutoka nchi makanisa wanachama wa UEM. Ubadilishanaji wa watumishi ndai ya UEM kati ya mabara haya matatu Afrika, Asia na Ujerumani utapata ufadhilli mahususi kutoka UEM, kuonyesha ni kwa jinsi gani suala la kufanyakazi kwa pamoja linavyopewa kipaombele katika suala zima la udugu. Miradi ya namna hii inachukuliwa kama miradi ya ubunifu mkubwa na kwajili hiyo basi kwa siku zijazo miradi hii itakuwa na sifa ya kupata kibali cha UEM na kutambulika kama miradi muhimu katika kuujenga udugu (Tazama ukurasa wa 18). Tunapenda kuwatia moyo katika kujikita katika mwongozo huu unaoonyesha hatua mbalimbali za utekelezaji wa miradi ya udugu na kuwa tayari kuzungumza na sisi kwa ushauri wowote kwa kadri mtakavyoona inafaa.

# I. Nafasi ya (Wajibu wa) Fedha katika Udugu

## Mtazamo wa Ki-Indonesia

Ujerumani kuna msemo unaosema kwamba urafiki unamalizwa au unaharibiwa na pesa. Kwa waindonesia, msemo huu hauwezi kueleweka vema. Hii ni kwasababu kwa waindonesia msaada wa kifedha kamwe hauwezi kuharibu urafiki kati ya mtu na mtu. Kwa waindonesia hakuna mtu anayejisikia aibu yoyote kuomba msaada wa kifedha toka kwa ndugu, rafiki au kwa mtu yeyote pale anapokuwa na shida ya kifedha na anahitaji msaada. Jambo hili linaitwa adat yaani ni utamaduni. Kinyume chake, mtu anayekopwa fedha anajiona kama mtu anayeaminika na kuheshimika na jamii inayomzunguka. Wala hakuna ubaya wowote ikiwa aliyeombwa fedha hana uwezo wa kumpatia mhitaji kiasi chote anachokihitaji basil sehemu tu ya fedha inayohitajika, wala hakuna shida yoyote ikiwa hawezi kabisa kumsaidia kiasi chochote mhitaji kutokana na kutokuwa na fedha ya kumsaidia mhitaji huyo. Isipokuwa ni vigumu kumpa mtu msaada wa fedha yule ambaye hatoki kwenye jamii moja na mwenzake. Ni kutokana na hali hii, msaada au mshikamano baina ya watu wasio wa jamii moja huwa hauna nguvu.

Kwa Ujerumani, hali ni tofauti. Mtu anasita kuomba msaada wa kifedha hata kutoka kwa ndugu yake, achilia mbali jirani. Hata hivyo kumekuwepo na mshikamano unaozidi kukua nchini ujerumani kila wakati. Huenda hakuna nchi ya ulaya inayoishinda nchi ya ujerumani katika kutumia uchumi wake mwingi katika kutokomeza matabaka ya watu, (walionacho na wasionacho) sehemu mbali mbali za ujerumani yenye, ulaya na duniani kote kuititia mpango wa misaada ya maendeleo.

Makanisa na sharika mbalimbali nchini Ujerumani viko mstari wa mbele katika kusaidia jumuiya za makanisa duniani na mitandao mbalimbali katika kuwezesha miradi mbalimbali ya maendeleo duniani. Lakini jambo moja kubwa linaloambatana na hili ni kwamba kila kitu kinatakiwa kupangwa na kutekelezwa kufutana na makubaliano kati ya wahusika, na kwa uwajibikaji wa hali ya juu. Katika hali nzima ya umoja wao, bado Ujerumani inaonekana kukosa sera katika ushirika na kwa upande wa washirika wake kunakosekana utaratibu wa namna ya kufikia malengo. Wasamaria wema wengi wa kijerumani, wanataka siyo tu kumsaidia mtu aliyeumizwa kando ya barabara, bali pia kumwonyesha mtu huyo njia sahihi ya wokovu. Siyo tu kwamba wajerumani wanataka kumpeleka hospitalini mtu yule aliyeumizwa, bali pia wanataka kudai kupatiwa bima ya afya inayostahili. Kwa upande wa udugu

baina ya makanisa pia, wajerumani wanapenda kuweka sera mbalimbali zinazohusu usimamizi na udhibiti wa mipango mbalimbali. Hii inaweza kuwa mzigo mzito kwa baadhi ya makundi ya udugu na hata kusababisha mvutano baina yao. Kumetokea kwa upande wa makundi ya udugu kutoka ujerumani yakidai si tu taaarifa ya matumizi ya fedha za miradi ya udugu kama jambo muhimu, bali pia yakiingilia mambo ya ndani ya kanisa la udugu bila kuombwa kufanya hivyo na kaniisa husika, wakati kanisa la ujerumani lenyewe lisinge-penda wala kuruhusu kuingiliwa kwa kiasi hicho.



Utofauti wa tamaduni na desturi baina ya makundi ya udugu ndiyo sababu ya kuwepo kwa matarajio tofauti juu ya lipi linafaa kwa udugu na lipi halifai katika udugu, pamoja na utofauti katika namna ya utendaji katika mambo yahusuyo udugu. Utofauti huu kamwe hausababishwi na tofauti za kitheologia baina ya makundi ya udugu. Kutambua uwepo wa utofauti wa mitazamo baina ya makundi ya udugu, hakupanui uelewa au upeo wa mtu binafsi tu, bali pia kunalisaidia kanisa katika kukabiliana kwa usahihi na changamoto zinazoikumba dunia yengetamaduni mchanganyiko. Ni kwa njia hii kanisa linaweza kutoa msaada stahiki, ulinzi na mwongozo kwa wahitaji. Udugu ndani ya umoja wa makanisa, hususani katika ugawaji na usambazaji wa fedha kama rasilimali, ni elimu ya kipekee kwa ulimwengu wetu tata na uliosambaratika. Hapa chini kuna orodha ya mambo matano muhimu kwa mambo yahusuyo ushirikiano kwa mambo ya kifedha katika udugu.




1. Kanuni za kimataifa na kiikumene zinazohusu fedha, kama vile uwazi na uwajibikaji, zinapaswa kuzingatiwa ipasavyo. Hii inamaanisha pia kwamba makubaliano yoyote ya kiutendaji na kiutekelezaji yaliyokubaliwa katika vikao husika au ngazi za uongozi au utawala ni lazima yajulishwe kwa watu wote au wahusika wote. Pia taarifai juu ya mwenendo mzima wa mradi (namna mradi unavyoendeshwa au unavyoendelea) nilazima iwafikie watu wote kwa uwazi na mwenendo mzima wa mradi usikinzane na lengo au kusudi la kuanzishwa kwa mradi huo.

2. Ni lazima kutofautisha kati ya miradi, shughuli za maendeleo (program) na huduma za msingi za kanisa mfano misioni na diakonia. Miradi ni jambo jema kwa udugu, ili kuanzisha au kuwezesha kuanzishwa kwa shughuli mpya ambayo ni muhimu na italifaa kanisa husika. Lakini ikiwa kwa angalao miaka mitano kanisa husika halitauchukua mradi huu na kufanya kuwa moja ya huduma zake za msingi, hivyo kushindwa kutoa mchango ufaao katika uendeshaji, basi mradi huu utachukuliwa kuwa haufai na utatikiwa kufutwa kabisa. Miradi inatakiwa ilisaidie kanisa la udugu ili liweze kuongeza ufanisi katika huduma zake za msingi kwa jamii na siyo kulifanya kanisa husika kuwa tegemezi na mambo mengine yanayofanana na hayo. Utegemezi wa kudumu wa fedha toka sharika au kanisa la udugu, siyo maana halisi ya udugu hata kidogo. Sharika au makanisa ya udugu nilazima yasaидiane katika nyakati za shida au uhitaji, lakini baadaye sharika hizi au makanisa haya yanapaswa kuchangia kwenye shughuli hizo zote kwa usawa.

3. Hitaji la kifedha kwaajili ya miradi linapojitokeza, nilazima kujua utamaduni wa pande zote zinazohusika katika udugu. Ili pande zote husika ziweze kujenga imani kila mmoja kwa mwenzake, basi ni jambo la maana sana kuhakikisha kwamba mradi pendekezwa unatokana na mawazo ya washarika wote. Mradi uwe ni makubaliano yaliyofikiwa na washarika wote baada ya kuwa na muda wa kutosha wa kujadili nini hitaji lao la msingi. Kukiwepo mtu ye yote, ambaye amebeba jukumu la kuwa daraja kati ya wahusika, mtu huyo anatakiwa awe amekwishakuzungumza na washarika juu ya mradi wanaoutaka na mapendekezo mengine yanayohusu mradi huo. Usawa unatakiwa hasa katika suala la majukumu ya pande zote husika kwa mradi pendekezwa, na makubaliano haya yanatakiwa yawekwe kwenye maandishi. Ikiwa kuna utata wa jambo lolote -iwe ni katika mjadala juu ya mradi au hata ikiwa ni utata katika matumizi ya lugha au maneno, basi ni jukumu la mtu huyu anayesimama kama daraja, kujipa muda wa kutosha na hata kuwahusisha wataalam wa lugha ili waweze kutafsiri ipasavyo na kuuondoa utata kabla makubaliano hayafikiwa. Ni muhimu kwa pande


husika kujipa muda wa kujadili kwa kiina juu ya mradi wanaouhitaji kabla ya kufikia makubaliano ya msingi. Kabla ya kufikia hitimisho au maamuzi ya mwisho, nilazima makubaliano haya yote yafikiwe kisheria na kuwekwa kwenye maandishi.

4. Ushirikiano wowote wa kifedha kati ya wadugu, unyaweka mambo ya msingi kwenye majaribu makubwa. Mambo hayo ni kama uaminifu, heshima, na upendo kati ya wadugu. Lakini ieleteke kwamba kwetu sisi tulio wafuasi wa Kristo, neno la Mungu linatufundisha kwamba hata wanafunzi wa Yesu hawakuwa watu wasio na dhambi. Nafasi ya fedha au kazi ya fedha, nguvu ya fedha na athari za fedha kwa maisha ya kanisa la Mungu, si mambo ya kupuuzia. Ikitokea mambo yahusuyo fedha yakafanyika pasipo mipango madhubuti, waliopewa dhamana ya kuwa mawakili wa fedha wanaweza kuzitumia fedha kwa kujinufaisha wao binafsi na siyo kwa malengo yaliyokusudiwa (Kufuja pesa). Lakini kwa upande wa watoaji fedha, pia kuna hatari ya kuingiwa na kiburi cha kujiona wao ni bwana wakubwa (watoaji) na wengine kuwa bwana wadogo (wapokeaji). Lakini ieleteke kwamba kiburi ni dhambi tu kama dhambi ya ufujaji wa fedha. Kukiwepo na ushawishi wowote kwa udugu, umaotokana na nguvu ya fedha ya watoa msaada, hasa unaopelekea wanaopokea fedha kuttakiwa na mtoa fedha kufanya hata lile wasilolitaka, jambo hili liwekwe wazi na lishughulikiwe ipasavyo na pande zote zinazohusika lakini kwa moyo wa upendo. Lakini pia kwa wale wanaotumia fedha za miradi kujinufaisha wenyewe au wanaofuja fedha za miradi, washughulikiwe ipasavyo kwa kufuata kan-



uni za kanisa husika. Na wale ambao wamejaa kiburi na kujiona kuwa bora zaidi ya wengine kwasababu ya fedha watoazo, nao waitwe na kuonywa ili waweze kubadilisha mienendo yao. Ni hapo haya yote yanapofanyika bila kukoma tena yakifanyika kwa upendo pasipo kumwaibisha mtu, faida ya udugu itaonekana na wala udugu hautaathirika wala kuharibika.

5. Ninapenda kutumia neno hili la kiingereza "centrifugal" kama msingi wa hoja yangu hii ninayotaka iwe hitimisho la mapendekezo yangu. Centrifugal inam-



aanisha nguvu ya mwendo wa kitu unatoka katikati kwenda pembedi. Hii ni kinyume cha centripetal, ambapo nguvu iliyopo katikati inazivuta nguvu zote za pembedi ziende katikati. Misioni au huduma ya Yesu Kristo ni centrifugal: ni Yesu mwenyewe anayewatuma wanafunzi wake waende ulimwenguni kote kuitenda kazi yake. Miradi ya Udugu kama ilivyo misioni na huduma ya Yesu Kristo, nilazima iwe centrifugal. Miradi hii isijibu swal la-nini tunaweza kufanya kwaajili yetu sisi binafsi, bali ilenye kujibu swal hili: Nini tunaweza kufanya kwaajili ya wengine? Miradi lazima ihudumie jamii nzima ya Afrika, Asia na Ujerumani na siyo kuhudumia tu wakristo wa makanisa ya Afrika, Asia na Ujerumani. Mungu analibariki kanisa lake ili kanisa liwe baraka kwa ulimwengu mzungu. Katika ulimwengu huu, Yesu Kristo anatuvuta twende kwake ili atutume kwenda ulimwenguni,

vivyo hivyo kupitia neno lake, Yesu Kristo anawavuta waafrika, waasia na wajerumani waende kwake.

Bwana Yesu anatubariki sisi na kututuma tukawe baraka kwa wengine, ili watu tunaotumwa kwao wawze pia kujifunza juu ya upendo mkuu wa Mungu ulio katika Yesu Kristo. Ikiwa tu fedha ya miradi inakuja katika mtazamo au uelewa huu, ndipo kama wakristo tunaweza kusema urafiki au udugu hauwezi kuharibiwa au kuvunjwa na fedha. Zaidi tutasema fedha inasaidia katika kupanua wigo wa marafiki..


#### **Sonia Parera-Hummel**

*Sonia Parera-Hummel UEM-kurugenzi ya Asia, mzaliwa wa Indonesia.*

## II. Namna UEM Inavyofanya

UEM inavyosaidia Miradi na Shughuli (Programu) Zingine

8




Ni mradi upi (eneo gani linastahili msaada) unaostahili ufadhili na ni vigezo gani vinatumika katika kupitisha mradi ili uweze kupatiwa msaada wa kifedha? Haya ni mambo muhimu yanayostahili kujadiliwa na makundi husika ya udugu kabla mradi haujaanza. Mwongozo juu ya kusaidia miradi na shughuli mbalimbali kwa makanisa yote wanachama wa UEM ilijadiliwa na kuitishwa kwenye mkutano mkuu wa UEM uliofanyika mwaka 2012. Mwongozo huo uliweka wazi vigezo katika kutathimini miradi na shughuli mbalimbali ndani ya UEM. Mwongozo huu ni kwaajili ya miradi yote na shughuli zote za UEM. Mwongozo huu ndiyo unaosaidia makundi yote ya udugu hususani katika masuala yahusuyo miradi mbalimbali baina ya pande zote zinazohusika.

Mwongozo unaohusu ufadhili kwaajili ya miradi pamoja na shughuli (programu) mbalimbali, umejengwa juu ya msingi wa kanuni zinazoongoza UEM amba zo ni zao la maamuzi ya mkutano mkuu wa UEM wa mwaka 2008. Kanuni yenyewe inasema: "Tunaamini kuwa misioni inahusu kumhudumia mwanadamu mzima (Kiroho na kimwili), hivyo tunahudumu pamoja ili ku-

timiza wajibu huu. Hii ndiyomaana tunachukulia uinjilisti, diakonia, utetezi wa haki za binadamu, maendeleo, na udugu kama msingi katika kueneza injili. UEM ni shirika la misioni la kimataifa, lakini linafanyakazi ndani ya nchi za Afrika, Asia na Ujerumani. Ili kuifanya kazi ya misioni kwa ufasaha, tunashirikiana na kugawana rasilimali na Baraka mbalimbali tulizonazo." Wajibu huu wa kumhudumia mwanadamu mzima kiroho na kiakili kwa kuweka mkazo katika uinjilisti, diakonia, utetezi wa haki za binadamu, maendeleo na udugu, msingi wake ni Injili kama ilivyoandikwa na Luka Mtakatifu 4:18-19 "Roho wa Bwana yu juu yangu, kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenitura kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwa. Na vipofu kupata kuona tena, kuwaacha huru waliosetwa, na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa."


## Maeneo Matano ya Huduma za UEM



### Uinjilisti

Tunaamini kuwa injili ni uweza wa Mungu uletao wokovu na upya wa maisha kwa mwanadamu, hivyo basi...


- ... tunaungana wote kwa pamoja katika kutiana nguvu katika maisha yetu ya kiroho, huku tukianzisha na kuendeleza miradi yoyote inayohusu huduma za uinjilisti kama jitihada za makusudi za kuwfikia watu wote kwa injili ya wokovu na kuwavuta ili waweze kumwamini Bwana Yesu
- ... tunaendeleza na kuwezesha shughuli mbalimbali (programu) zinazofanywa kwa umoja
- ... tunaendeleza na kuwezesha mipango mbalimbali (program) inayohusu ubadilishanaji wa mawazo kwa watheologia
- ... tunawahamasisha na kuwawezesha wakristo wa makanisa yote wanachama wa UEM kujifunza njia mwafaka za namna ya kuweza kufungua milango ya mazungumzo yahusuyo imani yao baina yao na watu wa imani zingine.



### Diakonia

Tunakiri kuwa wanadamu wote wameumbwa kwa mfano wa Mungu, hivyo basi...


- ... Tunaendelea kuimarisha mtandao hadi ngazi za chini kabisa (kaya) katika kupambana na ugonjwa wa UKIMWI (HIV na AIDS), kuwashudumia watoto yatima, wajane na wagane, na kuwashudumia waathirika
- ... Tunajibidisha katika kuhakikisha kuwa tunaboresha hali za maisha ya watu, hasa wale wenye mahitaji maalum
- ... Tunajibidisha kuboresha huduma za afya ili kuhakikisha kwamba tunaboresha huduma za afya ya mwili na kisaikolojia kwa watu wote
- ... tunasaidia makanisa yanayoendelea kuwashudumia watu waliokumbwa na maafa yanayotokana na sabbu za kiasili (natural disaster) au yanayosababishwa na watu (man-made disaster)



### Utetezi wa Haki za Binadamu

Tunaamini ya kwamba wanadamu wote wameumbwa kwa mfano wa Mungu na kwahiyo basi utu na haki yao haviwezi kuchukuliwa na mta yeyote, hivyo basi...


- ... Tunaheshimu na kutetea haki za binadamu
- ... Tunasaidia jitihada mbalimbali katika kutatua migogoro kwa njia za amani
- ... Tunashirikiana kuongeza nguvu katika jitihada zinazojikita katika kuleta usawa wa hali ya kiuchumi baina ya watu (kuondoa tabaka katika jamii) pamoja na jitihada za kuhakikisha kuwa dhana ya uongozi bora inapata nafasi/inaheshimika
- ... Tunajibidisha katika utunzaji wa mazingira



### Maendeleo

Tunaamini kuwa upendo wa Mungu unaendelea kuwawezesha watu, hivyo basi ...

- ... Tunasaidia na kuwezesha mipango (programu) mbalimbali inayowawezesha wanaume, wanawake na vijana kujiletea maendeleo
- ... Tunatoa nafasi za mafunzo mbalimbali
- ... Tunatoa ufadhilli kwaajili ya masomo ya elimu ya juu ili kuyaongezea uwezo au ufanisi makanisa yote wanachama
- ... Tunachangia katika jitihada mbalimbali za kutokeza umaskini wa aina zote



### Udugu

Tunajua kuwa sisi sote tu viungo vya mwili wa Kristo, na kwahiyo basi...

- ... Tunajibidisha katika kuhakikisha udugu baina ya makundi mbalimbali na udugu baina ya makanisa wanachama unajenguka na kuimarika. Udugu huu unajengwa kwenye misingi ya kuheshimiana, kuthaminiana na uwazi. ... Tunawawezesha mipango mbalimbali ya kutembeleana baina ya viongozi, wataalam na kwa wale wanaofanya kazi za kujitolea (Volunteers)
- ... Tunaanzisha mtandao baina ya vikundi au makanisa ya udugu ili kuwezesha kuwepo kwa mahusiano na udugu wa kila namna kwa makundi mbalimbali

# Vigezo Vitumikavyo katika Uwezesha ji Ki-fed ha(ufadhili)

Makanisa yote na taasisi zake zote ndani ya UEM wanawajibika katika utekelezaji, usimamizi na utoaji taarifa ya miradi. Miradi yote pamoja na mipango (programu) mbalimbali ya maendeleo, vinatakiwa kukidhi vigezo vifuatavyo:

10

## Kubeba Ushuhuda

Miradi na shughuli yoyote inayowezeshwa na UEM lazima ibebe ushuhuda kamili wa injili ya Yesu Kristo; iwe ni ile inayoalika wengine wamjue Kristo, inayopeleka uponyaji na inayoleta mshikamano baina ya watu.

## Kuongeza Uwezo/Ujuzi

Kuongeza ujuzi na kuongeza uelewa katika mambo ya ki-theologia, ki-misioni na ki-diaconia na miundombinu ya makanisa wanachama wa UEM ndiyo sababu kuu ya UEM kuwezesha miradi na shughuli mbalimbali za makanisa wanachama

## Ushiriki na Uwezesha ji

UEM inathamini watu wanaojituma au wanawajibika, na kwaajili hiyo UEM inawaweze sha watu hao wanaoweka jitihada katika kutambua na kuziweka wazi changamoto mbalimbali zinazowakabili na kutafuta njia za namna ya kupambana na changamoto hizo kwa kutumia uwezo walionao.

## Kutokomeza Ubaguzi

Shughuli mbalimbali za maendeleo pamoja na miradi vyote vinavyofadhiliwa na UEM, vinatakiwa viwalenge watu wote bila kujali dini zao, imani zao, jinsia, umri, asili au kundi nyonge au dhaifu analotoka mtu.

## Usawa wa Jinsia

Katika miradi ya udugu, suala la jinsia lazima litazamwe kwa umakini. UEM inapenda kuwepo na usawa wa jinsia kuanzia hatua za kubuni, kupanga, kutekeleza, na kutathimini miradi. Ieleweke kwamba usawa wa kijinsia ni moja ya vigezo muhimu vinavyotakiwa kuangaliwa kundi husika linapotoa maelezo juu ya faida zinazotegemewa kuletwa na mradi au shughuli (programu) inayoombewa ufadhili.

## Mradi Endelevu

Ufanisi endelevu (wa muda mrefu) au matokeo endelevu ya mradi au shughuli yoyote ya maendeleo, ni moja ya vigezo vinavyowezesha mradi au shughuli husika kupatiwa ufadhili. Hii inaonyesha kuwa mradi au shughuli husika imegusa miyo na maisha halisi ya walengwa kiasi ambacho walengwa hawa wanaweza kuyatumia matokea ya mradi au shughuli hii kwa mambo mengine kwenye maisha yao hata baada ya mradi au shughuli husika kufikia ukomo. Uwezesha ji amba ni matunda ya mradi uliofikia ukomo, unaweza kutumika kwa miradi mingine au kwa huduma zingine kwenye maisha ya wahusika.

## Utunzaji wa Mazingira

Kutokana na UEM kuwa na dhamira ya kuheshimu haki, amani na uadilifu kwa uumbaji, kila mradi au shughuli yoyote ya maendeleo, ni lazima iangalie suala zima la utunzaji wa mazingira.

## Tamaduni za Wenyeji na Rasilimali

Tamaduni na dini za wenyeji wa mahali ambapo miradi inafanyika, lazima viheshimiwe. Wenyeji wanatakiwa kuchangia rasilimali pamoja na ujuzi wao kwa mradi. Mchango wao unaweza kuwa katika mambo yahusuyo utatuizi wa matatizo mbalimbali lakini pia wanaweza kutumia njia mbalimbali katika kuchangia maendeleo ya jamii husika katika mambo yahusuyo maendeleo ya kiimani, kijamii, na kiuchumi kwa wakati wote mradi unapokuwa ukiendelea kwenye eneo lao.

## Miradi ya Umoja

Kushirikiana katika utekelezaji wa miradi au shughuli zozote za maendeleo hasa kwa makanisa wanachama wa UEM wa sehemu moja ni jambo la maana sana linalopaswa kuungwa mkono na hata kuendelezwa. Lakin pia ufadhilli unatakiwa pia kutolewa kwa miradi mingine na shughuli za maendeleo zinazofanya kwa ushirikiano baina ya makanisa wanachama wa UEM na makanisa mengine yasiyo wanachama wa UEM, au na jamii za dini nyingine, mashirika mengine ya maendeleo na mashirika ya maendeleo yasiyo ya kiserikali (NGO) yanayoendesha shughuli za maendeleo katika eneo husika. Hatahivyo mapendekezo ya miradi kama hiyo nilazima yapelekwe UEM na makanisa au taasisi za kanisa wanachama wa UEM.

## Vita dhidi ya Rushwa

UEM inapinga rushwa ya aina yoyote ile, kwani rushwa inabomoa misingi ya udugu wetu na inahatarisha ufanisi wa miradi na shughuli mbalimbali za maendeleo. Kanuni za UEM zinazokataza na kuzuia rushwa huku zikisisitiza uwajibikaji na uwazi ni mambo ya lazima ya kuzingatiwa katika ufadhilli wa miradi na shughuli mbalimbali za maendeleo. Kanuni hizi zinapatikana hapa: ([www.vemission.org/Code of Conduct against Corruption and for Transparency](http://www.vemission.org/Code of Conduct against Corruption and for Transparency))

## Uzuiaji wa Unyanyasaji wa Kijinsia

UEM haikubaliani na unyanyasaji wa kijinsia wa aina yoyote ile, bila kujali mahali unyanyasaji huo ulipofanyika. Kanuni zinazohusu katazo la unyanyasaji wa kijinsia ([www.vemission.org/ Code of Conduct against Sexual Harrassment](http://www.vemission.org/ Code of Conduct against Sexual Harrassment)) zinatakiwa kuzingatiwa wakati wote wa utekelezaji wa miradi na shughuli mbalimbali za maendeleo zinazofadhiliwa na UEM.

Wakati wote unapopanga mradi wako, uhakikishe ume-soma mwongozo huu na yule unayetegemea kushirikiana naye kwenye mradi pendekezwa, ili kuona ni vigezo gani vinahitajika kwa mradi unaopanga kuuombea ufadhilli na kuutekeleza. Ikiwa kuna vigezo vimesahaulika kuingizwa kwenye mpango wa mradi wako, angalia kama kuna uwezekano wa kuviiingiza. Kwa vigezo vyote mtakavyokuwa mmekubaliana na msririki wako, hakikisha vimeingizwa kwenye maandishi. Hii ni njia mojawapo inayoweza kukuwezesha kwenye mchakato wa kusimamia, kufuutilia na hata katika kutathimini mradi husika ili kuona ni vigezo gani vya ufanisi mlivyofikia na ni vigezo gani vinavyodai jitihada zaidi ili kuvifikia.

*Maeleo haya yanapatikana kwenye: The UEM Approach to Supporting Projects and Programmes, 26 October 2011*

# III. Hatua Mahususi za Kufikia Mradi Kamili

## Kuanzia Wazo hadi Utekelezaji wake

12

Sura hii inaelezea hatua mbalimbali za mradi, kuanzia wazo juu ya mradi, utekelezaji wake na mwisho ni hitimisho au ukomo wa mradi. Maelezo haya yanaweza kutumika kama mwongozo au njia inayoweza kutumika katika kupanga hadi kuuwasilisha mradi kwa UEM. Hata hivyo ni muhimu kuzingatia mazingira ya mahali mradi unapofanyika.

### Mradi ni nini?

Mradi ni:

- Kilichopangwa mahususi kwa walengwa;
- Kilichopangwa kwa kuzingatia wakati muafaka na rasilimali;
- Pendekezo lenye upekee wa aina yake;
- Pendekezo lililo na mwanzo na pia ukomo wake (lenye wakati au kipindi maalum).

Shughuli za maendeleo (programu) ni tofauti na miradi. Hizi ni zile shughuli zote za maendeleo zilizokusudawa kufanyika kwa kipindi kirefu na haziwekewi muda maalum wa kufikia ukomo ambapo rasilimali zake zietalekezwa kwenye matumizi mengine. Miradi inaweza kubuniwa kutokana na shughuli au program za maendeleo zinazoendelea na wakati huohuo shughuli za maendeleo au program zinaweza pia kutokana au kuwa matokeo ya uwepo wa mradi inayoendelea.

### Hatua Muhimu kwa Mradi

#### 1. Wazo la Mradi, Hatua ya Mwanzo

Kuna wakati mradi unaweza kubuniwa ghafla kutokana na wazo kuzaliwa wakati watu flani wakiwa ziarani mahali flani. Hatahivyo kabla ya kuanza kuutekeleza, ni vema kuwepo na majadiliano na watu mbalimbali juu ya wazo hilo la mradi pendekezwa. Maswali yaliyoorodheshwa hapa chini yanaweza kusaidia katika kuhakikisha wahusika wote wameshirikishwa kikamilifu katika kulijadili wazo pendekezwa. Watakuwa wamepata nafasi ya kutosha ya kujadili na kuchambua matatizo mbalimbali yanayowakabili na njia za kutatua matatizo hayo.

Njia makini ya namna ya kujadili wazo la mradi inasaidia katika kufikia uwamuzi wa busara juu ya mradi unaofofaa, hivyo kuufanya mradi utekelezwe kwa mafanikio.

**a** Lipi ni tatizo linalotukabili na ni malengo gani tunayotaka kuyafikia kuptita mradi tunaotaka kuupendekeza? Iwe kabla ya wazo au hata baada ya kuwa na wazo juu ya mradi mnaotaka kuutekeleza, ni vema

kwanza kuwa na muda wa kutosha kujadili kwa kina juu ya matatizo ambayo mnataka yatatuliwe kuptita mradi mnaotaka kuupendekeza. Kwa kawaida kunakuwa na njia mbalimbali za namna ya kutatua tatizo, hivyo ni vema kuwa makini katika kujadili hoja mbalimbali zihusuzo mradi katika hatua hii.

**b** Nani wahusika wakuu wa mradi? Hapa ni vema kuweka wazi nani wahusika wa mradi na nani ni walengwa wa mradi husika. Walengwa ni lazima washirikishwe kuanzia mradi unapoanza. Inawezekana pia kwamba walengwa wa mradi wanaweza kuyaelezea matatizo yao tofauti na watu wengine wanavyoyaelezea (watazamaji).

**c** Rasilimali gani ipo mahali hapo? Kusudi la swalii hili si kuanza kufanya mahesabu ya gharama ya mradi, bali ni kukusanya mawazo juu ya wapi rasilimali itapatikana kwaajili ya mradi unaotakiwa kufanywa. Si lazima rasilimali zinazouliziwa ziwe fedha, hapana, bali yaweza kuwa vifaa au nguvukazi kwaajili ya mradi. Kila anayehusika na mradi anatakiwa achangie rasilimali kwaajili ya mradi husika.


**d** Ni kwa namna gani tunapima matokeo ya mradi? Ni wakati gani na kwa njia gani tunajua mradi umefanikiwa au umetekelezwa kwa ufanisi? Ni vema kutathimini mradi ili kuona kama moyoni mwenu mmeridhika na ufanisi mlionfiki, na si kwa kuangalia sana vipimo mlivyojiwekea kanakwamba ni sheria au kanuni zisizweza kubadilika. Kwa mfano mnaweza kuamua kwamba lengo mojawapo la mradi, hususani katika tathimini, ni pale ambapo kila mmoja wa washiriki atardhika na ufanisi uliofikiwa. Hata hivyo ni vema jambo hili likawekwa kwenye orodha ya malengo tarajiwa, hata kama hiyo inaeleweka na kila mshiriki katika mradi.

#### 2. Tathmini ya Hali ya Mahali Mradi Unapokusudiwa Kufanyika

Mara wazo la mradi linapokuwa limefikiwa, kinachofutia ni kufanya tathmini ya hali ya mahali ambapo mradi unakusudiwa kufanywa. Hakuna maamuzi yoyote yanayotakiwa kufikiwa kabla ya kufanya jambo hili muhimu linalohusisha tathmini ya mambo mbalimbali yatakayopelekea kujuwa hali halisi ya mahali hapo na mazingira ya mahali hapo kwa ufasaha Zaidi.

**a** Ni nani hasa au ni kundi gani hasa linalolengwa na mradi husika? Hali ya maisha ya watu wa mahali hapo na mahitaji yao ni mambo yanayotakiwa kufanyiwa upembuzi yakinifu kwa ufasaha na kwa uhakika bila

## Mzunguko wa Mradi: Hatua Mbalimbali za Mradi



kukosewa. Kuwasikiliza walengwa ni jambo lenye umuhimu wake wa pekee katika hatua hii, na siyo kukurupuka katika kutoa majibu ya shida za walengwa.

**b** Mazingira ya jamii husika yakoje? Swali hili linaam-batana na maswali yafuatayo:

- Je hali ya kisiasa na kijamii kwa ujumla ikoje mahali hapo (ni ya namna gani)?
- Je kuna wadau wengine wa maendeleo wanaotoa huduma na kutekeleza miradi mahali hapo?
- Je kuna wadau wengine ambaao wanauzoefu na wazo hili la mradi tarajiwa?
- Je ushirikiano una mantiki yoyote?
- Nani ni mlengwa wa mradi?
- Je kuna ye yote atakayeathiriwa (atapata hasara) kuto-kana na mradi pendekezwa? Kama jibu ni ndiyo, je kuna haja ya kubadilisha wazo la mradi?

**c** Mambo ya Kisheria/ Viwango /Vigezo viliviyowekwa na serikali

Ni muhimu kujua na kufuata vigezo na viwango vya serikali ya mahali ambapo mradi utaananzishwa. Vigezo vinaweza kuhusisha hati miliki ya mradi husika, sheria zinazohusiana na upimaji na ujenzi wa majengo na masharti mbalimbali ambayo yasipozingatiwa yanaweza kuathiri mradi. Unatakiwa pia kufanya utafiti ili kujua wajibu wa serikali katika utekelezaji wa mradi tarajiwa. Na ikiwa kuna msaada wowote ni vema kujua ni msaada wa namna gani ambaao utatoka serikali ili kuuendeleza mradi huu.

**d** Je mambo yote yahusuyo mradi yako wazi au kuna masilahi ambayo bado hayajadiliwa kwa uwazi? Je kuna malengo yaliyofichika au ajenda iliyojificha nyuma ya mradi huu?

**e** Mawasiliano na Kanisa kwa ujumla ni jambo la muhimu:

- Je kanisa zima limehusishwa au je limepewa taarifa juu ya mradi tarajiwa?
- Je kuna mtaalam wa miradi wa kanisa zima ambaye amehusishwa kwenye upangaji wa mradi tarajiwa?
- Je kuna uzoefu wowote juu ya mradi kama huu uli-opendekezwa au unaotarajiwa kuanzishwa?

**f** Je mradi tarajiwa una uhusiano wowote na shughuli za udugu? Je ni jambo ambalo linamvuto kwa watu wa jamii ambapo mradi utaananzishwa? Je jamii husika itahamiska katika kushiriki kwenye utekelezaji wa mradi husika?

### 3. Malengo

Kuyaweka malengo yote kwa usahihi na ufasaha ni jambo la lazima:

**S** Lazima kuwepo na lengo maalum: Lengo hili lazima liwe wazi na sahihi.

**M** Lengo au malengo lazima yawe ni yale yanayoweza kupimika au kupimwa na vigezo lazima viwepo vya kupima kama malengo yamefikiwa au la.

**A** Lazima malengo yawe yamekubalika na washiriki wa mradi: Washikadau wote wa mradi pamoja na walengwa lazima wakubaliane juu ya malengo ya mradi wao

**R** Malengo lazima yawe halisia: yawe ni malengo yale yanayoweza kufikiwa

**T** Lazima kuwepo na muda maalum wa mradi: Lazima kuwekwa muda mahususi wa utekelezaji wa mradi husika

Kwa maneno mengine, hii inamaana kwamba malengo yanayotakiwa kuwekwa bayana, yanayolenga kufikia ufanisi au matokeo ya mradi yanayoweza kupimika, ni budi yawe yamekubalika na kuitishwa na pande zote zinazoshiriki katika mradi, yawe ni malengo yanayoweza kuhakikiwa au kufanyiwa upembuzi yakinifu kwa urahisi kwa kuwatumia wataalam na rasilimali zilizopo, na yawe ni malengo yanayoweza kufikiwa ndani ya muda uliopangwa wa mradi husika. Kunatakiwa kuwepo malengo ya jumla ya mradi na pia yawepo malengo madogo madogo yanayoweza kutathminiwa hatua kwa hatua. Kwa malengo yote, lazima kuwepo na viashiria pamoja na muda maalum uliowekwa kwa ufuatiliaji wa hatua mbalimbali za mradi. Kuwepo na ufuatiliaji na kufanya tathmini ya mwenendo mzima wa mradi ili kuona kama kuna mabadiliko yoyote katika mwenendo mzima wa mradi. Viashiria hivi nilazima vionyeshe wazi kama malengo ya mradi yamefikiwa au la.

Jambo muhimu hapa ni umuhimu wa kushirikishana juu ya malengo, tena yaandikwe, na kuhakikisha kila mdau wa mradi anaona malengo haya kama malengo yake. Kama hauna uhakika kama jambo hili limeeleweka sawasawa, tafadhali tafuta nafasi ya kukutana na wadau wote wa mradi kisha jadiliana nao kwa ufasaha juu ya mambo yote hususani malengo ya mradi na hatua zake. Hapo ndipo umiliki wa mradi unapojidhi-hirisha. Kukubaliana kwa dhati katika malengo ya mradi, kunawezesha mradi kuendelea kwa ufanisi.

SWOT ni njia tata inayotumika katika kufanya tathmini, lakini yenyeefaida kubwa kwa mradi. Ni njia inayoweza kuibua fursa ambazo hata hazikufikiriwa kabla ya SWOT. Lakini pia njia hii ya tathmini ya SWOT inaleta nuruni udhaifu na vikwazo katika uendeshaji wa mradi. Kwahiylo njia hii inasaidia kuonyesha matatizo ya mradi mapema:

Tathmini kwa njia ya SWOT inahusisha malengo yali-yokwisha kuwekwa bayana.

Ni kwa namna gani tathmini ya SWOT inafanya kazi:  
Tunaweka kipaombele kwenye mambo ya ndani au hali ya ndani:

Tunakusanya nguvu zinazofanya malengo yafikiwe  
Kitu gani tunachoo?

Kitu gani tunauwezo nacho?

Nguvu yetu au uwezo wetu uko kwenye nini?

Tunaweka kipaombele kwenye madhaifu ya ndani

Maswali muhimu ni:

Udhaifu wetu uko kwenye nini?

Vitu gani na wapi tumepungukiwa?

Zipi ni changamoto zinazotukabili/zinazotuzunguka?

Kwenye hatua ya pili, tunaweka kipaombele zaidi kwenye mambo yaliyo nje yetu:

Hapa tunachunguza fursa za nje:

Hili jedwali linaweza kuleta au kupelekea matokeo muhimu katika kupanga mradi

### Yenyemsaada

#### Mafanikio/Uwezo

**M**


### yenyemadhara

#### Udhaifu

**U**

Ndani

Nje



Nani anaweza kutusaidia?  
Wapi tunaweza kukimbia au kutegemea?  
Fursa gani zipi kwa wakati huu?

Hatua ya mwisho ni ya kuorodhesha maendeleo yasi-yofaa na hatari:

Ni vikwazo gani kutoka nje vinavyoweza kukwamisha?

Nani anatuzuia kutimiza tunalotaka kukusudia (nji-anji)?

Ni hatari zipi tunaweza kuzitaja?  
Hali zipi zinaleta vikwazo?

## 4. Makubaliano ya Mradi

Msingi wa mpango wa mradi wako upo kwenye mambo yote ya mwanzo kama yalivyoelezwa hadi kufikia hatua hii, matokeo ya tathmini ya hali halisi na ikiwezekana, matokeo ya tathmini ya SWOT. Hatua hii inayou-fuata inahusu ugawanaji wa kazi na majukumu.

**Upangaji wa mradi lazima utoe pitcha ya mambo yafuatayo:**

- **Malengo ya jumla**
- **Malengo madogo-madogo, lini na kwa namna gani yatafikiwa**
- **Ratiba kamili**
- **Uwajibikaji: Ikumbukwe ya kwamba kundi la walengwa na nchi ambapo mradi unatarajiwa kuanzishwa watatakiwa kuwajibika ipasavoy kwa mradi. Hivi ndivyo wajibu kwa mradi unavyokua. Wale wote wanaowajibika kwaajili ya mradi lazima washirikishwe kwenye mradi husika.**

**• Mpango wa Upashanaji habari:**

Nani anahitaji kupeleka habari ya namna gani na kwa nani? Mpango uhusuo uhusiano wa umma (Public Relations) unahitajika.

**Mpango wa Fedha unatakiwa kuwa na mambo yafuatayo:**

Ratiba ya gharama sahihi, inayoonyesha lini gharama ya kitu gani itapanda

Inatakiwa ionyeshwe wazi ni gharama zipi za usimamizi wa mradi zitapanda (gharama za uendeshaji) na ni nani atalipa gharama hizo. Pale inapowezekana, mradi unatakiwa uzalishe pato litakalowezesha ulipaji wa gharama za usimamizi wa mradi. Gharama za usimamizi wa mradi hazitakiwi zilipwe na wafadhilli kipindi chote cha mradi husika. Mara nyingi gharama za usimamizi wa miradi, zinawenza kuzorotesha mwenendo mzima wa mradi hata

kuufanya usiweze kuwa endelevu, mfano shule inapojengwa lakini bila kubakiza fedha kwaajili ya kuwalipa waalimu.

Mpango wa ukusanyaji wa mapato lazima uwepo ili kuweza kukabiliana na gharama za usimamizi wa mradi. Inatakiwa asilimia angalao 20 ya gharama ya mradi itengwe na aliyesababisha mradi kuwepo; malipo ya namna hii yanaweza kuwa kwa njia na namna mbalimbali kama vile mali ya aina flani au wafanyakazi (watumishi wa mradi/nguvukazi).

Chunguza na kutathmini kama kuna uwezekano wa kushirikisha mashirika mbalimbali katika kusaidia gharama za mradi. Mfano wa mashirika hayo ni kama Mkate wa Dunia (Bread for the World) au ubalozi wa nchi mbalimbali wanaofanya kazi katika eneo ambako mradi husika umeanzishwa.

Kuwepo na mipango ya kutunisha mfuko wa miradi (harambee) na watu wapewe wajibu wa kuisimamia mipango hiyo. Fursa za ukusanyaji fedha zinajumuisha shughuli mbalimbali au skukuu mbalimbali za sharika, kutoa kwa hiyari, na kwenye sherehe au skukuu za kitamaduni. Vipeperushi, tovuti vyote vyenyemaelezo yanayohusu mradi, pamoja na huduma ya Uhusiano wa umma, hasa kuititia vyombo vya habari kama vile radio, TV, majarida ya sharika mbalimbali vya eneo husika vinaweza kutumika katika ukusanyaji wa fedha za mradi. Kuititia utoaji wa huduma za elimu kama vile darasa la kipaimara, au uuzaaji wa nguo za akima mama kama vile khanga au vitenge inaweza kuwa njia mojawapo ya ukusanyaji wa fedha lakini pia yaweza kuwa njia muhimu ya kuwezesha mazungumzo juu ya udugu kuendelezwa. Lakini pia ni jambo la maana sana kuweka wazi nani anahusika na utoaji risiti na shukrani kwa kila anayetoa mchango wake kwaajili ya mradi.

Maelezo haya yote (maelezo ya mradi kwa ujumla na mpango wa fedha) vinapaswa kuandikwa kama muhitasari, pamoja na mpango wa utekelezaji. Vyote kwa pamoja vипитishwe na kusainiwa na vyombo husika. Makubaliano kwa uwingi wa kura ni jambo la muhimu sana.

## 5. Utekelezaji wa Mradi

Baada ya kuwa mradi umekwishakupangwa, kinachofuatia ni utekelezaji wa mpango kazi ikifuatiwa na usimamizi wa mradi. Usimamizi wa mradi ni ushirikishanaji wa habari kwa usawa, mawasiliano mazuri, na kurekodi mwenendo mzima wa mradi.

### Maswali muhimu ni:

- Je tuko kwenye njia sahihi ya kutufikisha kwenye malengo tuliojiwekea?
- Je kuna maendeleo yoyote ambayo hatukuyaona mwanzo na yanayotutaka tufanye kitu au jambo flani la ziada?
- Je kuna mambo yoyote ambayo tulitathmini vibaya na kwamba sasa tunahitajika kuchukua hatua zingine za ziada?

Lengo la maswali hapo juu, si kubebeshana lawama kwa jambo au mambo mabaya yaliyojitekeza, bali ni kufanya wahusika waweze kusahihisha kwa haraka ikiwa kuna jambo bayo limejitekeza katika mwenendo mzima wa mradi. Mawasiliano ya kila wakati yanasaidea sana katika hatua hii, hasa ikiwa jambo hili lilikubaliwa na washiriki wote tangia mwanzo. Kwa kundi la

udugu linalofadhili mradi, ni vema kuwa makini katika kuhakikisha kama fedha inayotolewa inafanya kazi ili-yokusudiwa.

- Je wafadhili wanahitaji taarifa (ripoti) na je iandikwe kwa mtindo gani (iandikweje)?
- Wafadhili ni lazima wathaminiwe na kupewa taarifa juu ya mwenendo wa mradi.
- Fedha za mradi lazima ziende kwenye mradi. Hili lifanyike kuititia UEM kwenda kwenye kanisa husika ili kuzuia ufujaji wa namna yoyote. Watu wengi wakishirikishwa na kujua juu ya fedha za mradi, hatari ya kupotea kwa fedha hizo inapungua.
- Pande zote zinazohusika na mradi zinatakiwa kupata habari juu ya michango yoyote inayotolewa kwaajili ya mradi husika. Kukiwepo na tatizo lililojitekeza linalohusu upashanaji habari juu ya michango mbalimbali, basi pande zote zinazohusika zitafute uwezekano wa kujadili suala hili na kulitafutia ufumbuzi.

### Yafuatayo ni mambo muhimu kwa kundi la udugu lililopatiwa ufadhilli:

- Je mradi unaendelea kama ulivyokusudiwa?
- Je kuna mahali panaleta tatizo kwa mwenendo mzungu wa mradi?
- Je ni wapi pamekuwa na hatua nzuri na ya kuri-dhisha?
- Je kuna ukaguzi wowote wa mradi uliofanyika?
- Je tumeweza kupiga picha zozote za mradi, video fupi au hata mahojiano na wahusika juu ya mradi, vyote ambavyo tunaweza kuvituma kwa wafadhili kama maelezo yatokanayo na huduma ya ofisi ya uhusiano wa umma?
- Tuma taarifa zinazohusu maendeleo ya mradi pamoja na taarifa ya fedha

Ni muhimu kwa pande zote zinazohusika na mradi kuwasiliana kila wakati, kushirikishana mapema juu ya tatizo lolote, kusimamia mradi kwa njia ya uwazi, kila mmoja kuwajibika na kurekebisha jambo lolote jipyaa linalojitekeza. Pakiwepo na tatizo waweza kuomba ushauri wa mtaalam kutoka UEM ili asaidie katika kurekebisha kasoro inayojitekeza katika mwenendo wa mradi.

## 6. Ukomo wa Mradi, Tathmini

Lengo kuu la kufanya tathmini ni kuuchambua mradi na kuutazama kwa karibu kwa kuangalia ufanisi wake kwa mtazamo wa malengo yaliyokuwa yamewekwa na haya ambayo yamefikiwa na pia kuangalia jinsi mradi huo ulivyoendeshwa au ulivyotekelizwa. Kwa kifupi ni namna ya kutumia vigezo mbalimbali katika kupima thamani ya mradi. Lengo hapa siyo kuhukumu wala kunyosheana vidole kwa jambo lililokwenda vibaya, bali ni:

- Kupata ufahamu au ujuzi;
- Kujenga uwazi;
- Kujenga dhana ya Uwajibikaji (kwa wafadhili na wa-changiaji wengine walioshirikishwa);

- Mafanikio katika utoaji na utunzaji wa taarifa;
- na Zaidi ya yote, ni kujifunza kutokana na yaliyotokea!

Kutazama nyuma (yaliyopita) ni muhimu katika kuboresha hali ya sasa na ya baadaye.

Unaweza kufanya tathmini wewe mwenyewe au ukajiri wataalam wasio washiriki wa moja kwa moja wa mradi husika ili waifanye kazi hiyo ya kutathmini mradi. Imeonekana kwamba tathmini ya miradi yenye manufaa zaidi ni ile inayofanywa na wahusika wa mradi wakisaidiwa na washauri kutoka UEM makao makuu, au ofisi za kikanda za UEM kama vile Medan au Dar es Salaam, au ofisi za umoja wa makanisa.

Tathmini ya mradi lazima iwhausishe wahusika wote wa mradi husika bila kuwasahau walengwa wa mradi huo.

Mambo ya msingi katika tathmini ya mradi ni malengo yaliyowekwa na wahusika, mpango wa mradi na mpanago wa fedha, pamoja na matokeo ya usimamizi wa mradi.

#### **Maswali muhimu ni:**

1. Je malengo yetu yamefikiwa?
2. Je yepi ni matokeo ya mradi huu (yaliyokusudiwa na yasiyokusudiwa)?
3. Je mpango wa mradi pamoja na mpango wa fedha vilizingatiwa, au kulikuwa na mabadiliko (ya kawaida kutokana na sababu za msingi)?

4. Je ni mambo gani tunaweza kujifunza kutokana na utekelezaji wa mradi huu ambayo yanaweza kutusaidia katika kutekeleza miradi mingine?

Ni lazima iwekwe wazi juu ya nani atakuwa msimamizi wa mradi utakaofuata mbeleni. Ni jambo la maana sana ikiwa wajibu na kwa njia hiyo umiliki wa mradi unaelekezwa kwa nchi ambamo mradi umetekelezwa (ili wahusika wajisikie kuwa mradi ni mali yao). Jambo hili linaweza kuwa la msingi sana linalohitaji kufanywa waziwazi kupitia alama flani. Taarifa ya fedha ni muhimu ikaandalialiwa na nakala yake kutumwa kwa pande zote zilizoshiriki katika kuwezesha au kuufadhili mradi husika.

Hapa mwisho kabisa, kila aliyehusika au kushiriki katika utekelezaji wa mradi, anatakiwa aridhike kwa hatua ambayo imefikiwa. Ni muhimu kuandaa sherehe kubwa itakayojumuisha wasimamizi wote wa mradi, wafadhili na wengine wote waliochangia kwa namna yoyote ile katika kuhakikisha mradi unafanikiwa, ili kuwashukuru kwa kazi waliyofanya. Hii inaweza pia kuwa hamasa kwa wafadhili inapotokea unaomba ufadhilli kwa mradi mwingine mpya. Mradi unatakiwa kukabidhiwa, na kila mmoja apate nafasi ya kushangilia kwa kukamilisha mradi. Haya yote yanasaadid katika kuleta hamasa ya kubuni wazo jipya la mradi mpya.

# Kupanga

## Ushirikishaji wa walengwa

## Tathmini

**Kufanya marejeo kwa umakini sana na tathmini  
ya matokeo na mchango wa mradi**

LENKO LA KWANZA: Uwajibikaji na Usimamizi

LENKO LA PILI: Anzisha mchakato wa kujifunza na kutafakari

#### **Matarajio ya hali inayotegemewa na wengi na hatua za kufikia huko, huku ukizingatia mambo yafuatayo:**

1. Rasilimali na mazingira kwa ujumla
2. Kupima athari na kufikiri njia mbadala
3. Kuangalia fursa (kundi la walengwa, fedha, n.k.)

## Usimamizi

1. Kusanya uchunguzi na habari zote zinazoweza kusaidia katika usimamizi (data)
2. Chambua na kutathmini habari zote za uchunguzi
3. Fanya uwamuzi kuhusiana na udhibiti

#### **Namna mbalimbali za kufanya tathmini**

Tathmini ya ndani na/ au Tathmini ya nje  
Tathmini ya namna ya au muundo wa ufadhili

## IV. Kibali cha UEM kwa miradi ya Udugu

18



Wajumbe wa mukutano wa udugu uliofanyika Parapat, Indonesia (2012) waliweza kuchambua na kuyaweka wazi baadhi ya maswali ya maana yahusuyo upangaji wa mradi, usimamizi wa mradi na kufanya kutathmini ya mradi ndani ya UEM. Kwa mfano:

- Ni kwa namna gani mradi unaweza kubuniwa hata ukamhudumia mwanadamu mzima (kimwili na kiroho pia)? Je miradi inaweza kubeba ushuhuda wa injili hata iweze kuwavuta na kupelekea uponyaji vyote vikiashiria mshikamano?
- Ni kwa namna gani miradi inaweza kuchangia katika maendeleo na katika kuwawezesha watu?
- Miradi inamchangano gani katika kubadilisha kanisa na jamii?
- Miradi inamchangano gani kwa makundi yote ya udugu katika kila nchi?
- Ni kwa namna gani miradi yaweza kuwa endelevu?

Hiki kijitabu cha mwongozo juu ya miradi kimekwishakueleza juu ya mihimili mitano ya UEM am-bayo ni (1) uinjilisti, (2) maendeleo na uwezeshaji, (3) diakonia, (4) utetezi wa haki za binadamu katika masuala yahusuyo amani, haki na uadilifu dhidi ya uumbaji na (5)udugu (Tazama ukurasa wa 9). Baada ya kusema hayo, ieleweke kuwa kuichukulia miradi kama njia ya kumhudumia mwanadamu kimwili na kiroho na kuiona miradi kuwa ni mipango endelevu, ni mtazamo wenye historia ndefu ndani ya UEM.

Lengo la UEM ni kuifanya mbinu hii ya namna ya kupanga miradi ieleweke kwa ufasha zaidi kuliko ilivyo sasa, na kibali cha UEM kitasaidia kulifikia lengo hili. Kwa njia hii UEM inayakaribisha makanisa yote, majimbo yote na makundi yote ya udugu wanachama wa UEM, kuangalia kwa makini hatua mbalimbali za kupanga na kutekeleza miradi mbalimbali ya udugu. UEM inaamini kuwa kuna umuhimu wa kutumia mpango huu unaotekeleza miradi kwa kuzingatia mambo makuu matatu(kupanga mradi, Kusimamia mradi na kufanya tathmini ya mradi) kama kipimo mahususi katika utekelezaji wa miradi kwa uwazi na kuifanya iwe endelevu. Ili kupata kibali cha UEM kwa miradi ya udugu, waombaji wa mradi lazima kuhakikisha wanafaulu kukidhi vigezo vitano vinavyothibitisha kwamba mtazamo wa UEM kwa miradi ni: mradi umkomboe mtu mzima (kimwili na kiroho) na uwe endelevu.

### 1. Uamuzi wa Wadugu wote wanaoshughulika na mradi

Washiriki wote wa mradi wanafanya maamuzi ya namna ya kupanga mradi wautakao kuititia vikao vyao na kuhakikisha kwamba mradi unakidhi vigezo vilivyokubaliwa na UEM na kisha wanatuma maombi ya kupata kibali kutoka UEM kwaajili ya utekelezaji wa mradi wao. (hatua hii ni mfano wa kufuatwa kwa kila mradi unaoombewa kibali).

## 2. Ushirikiano au umoja katika upangaji na utekelezaji wa mradi

Mradi unapangwa na kutekelezwa kwa umoja au kwa ushirikiano baina ya makundi yote yanayohusika na mradi husika, na kisha kwa umoja au ushirikiano baina ya makundi hayo yote, mradi unafadhliliwa kwa fedha na hata kwa njia zingine mbalimbali nje ya fedha.

## 3. Upangaji wa mradi wenyewe mitazamo au vipaombele mbalimbali

Angalao mihimili miwili ya UEM kati ya mitano iwe dira katika kupanga mradi:

- Utetezi wa haki za binadamu (wa haki, amani, na uadilifu kwa mazingira)
- Uinjilisti
- Maendeleo
- Diakonia
- Udugu

Mradi wa namna yoyote unaokidhi viwango vilivyo okubaliwa, unaweza kupangwa na kutekelezwa kwenye nchi na kanda zote zinazohusika pale inapowezekana kufanya hivyo.

## 4. Uelimishaji

Sharika na makundi mbalimbali ya mahali ambapo mradi utaanishwa au unaendeshwa, mfano makundi ya vijana, wanawake, taasisi mbalimbali kama shule katika maeneo au katika nchi ambazo washiriki wa mradi wanaishi yanamchango mkubwa kwa mradi. Makundi haya yote kwa pamoja yanatakiwa kusaidia mradi kwa njia ya semina za uhamasishaji, warsha, makongamano na njia zingine nyingi zinazofanana na hizi.

## 5. Huduma za uhusiano wa umma (Public relations work)

Vyombo au ofisi za makanisa au vyombo visivyo vya dini lakini vinavyotoa huduma za uhusiano wa umma katika eneo ambapo mradi unaendeshwa, visaidie kueneza habari ya matukio yoyote yenye uhusiano na mradi unaoendelea mahali pale. Matukio hayo yaweza kuwa ni semina au shughuli zozote zile zenye lengo la kuhamasisha maendeleo ya mradi husika.

### Maombi ya Kibali cha UEM Kitengo cha Udugu

Mara baada ya kukidhi vigezo vitano vya UEM, na baa da ya mashauriano baina ya wahusika wa pande zote, maombi yanaweza kutumwa kwa barua au kwa barua pepe kwenye ofisi inayohusika nchini ujerumani, au Afrika au Asia. Kichwa cha habari cha barua hiyo kiwe: "Kibali cha Udugu." Mchakato mzima unaweza kuchukua muda wa hadi majuma nane kwaajili ya kufanya mapitio ya maombi husika. Ikitokea kuna maeleo yoyote yamekosekanana hivyo yakahitajika, ofisi yoyote husika ya UEM itakujulisha ili uweze kuwasilisha maeleo hayo yanayohitajika. Maombi yako yakiwa yamepitishwa na kuonekana yanakidhi vigezo vinavyohitajika, utatumwa kibali cha UEM. Tunashauri kuwepo na ibada maalum kwaajili ya tukio la kupatiwa au

kupokea kibali kwaajili ya mradi. Lakini pia uitumie nafasi hii kuwaeleza wanajamii kwa kinagaubaga (kwa uwazi) nini makusudi ya mradi na nini wanajamii wakitarajie kutoka kwenye mradi husika. Kibali ni halali kwa mradi huo mmoja uliokubaliwa. Makundi yote ya udugu yanaalikwa kuleta maombi kwaajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali.

## Kibali cha UEM kwa Miradi bora ya Udugu



### Mapendekezo kuhusiana na kibali cha UEM

- Kibali kinaandikwa kwa rangi zilizomo kwenye nembo ya UEM, kuonyesha kwa urahisi kwamba kibali hiki ni mali ya UEM.
- Namna ya rangi zilizomo kwenye kibali au nembo hii, zinawakilisha maeneo makuu ya UEM yaani Afrika, Asia na Ujerumani
- Alama ya aina moja iliyomo kwenye nembo ya UEM, inawakilisha usawa katika udugu
- Mtazamo wa udugu ndani ya UEM unawakilishwa na alama au maumbo kama yanavyoonekana kuungana ungana kwenye nembo ya UEM, na hii inaonyesha jinsi udugu ndani ya UEM ulivyo: maeneo haya makuu matatu ya UEM yanatazamana kuonyesha kwamba yanashirikiana na kusaidiana katika mambu mbalimbali
- Rangi ya tano ya kijivu inawakilisha mihimili mitano ya UEM: Utetezi wa haki za binadamu, diakonia, maendeleo, uinjilisti na udugu.
- Kwenye nembo hii kuna maumbo yaliyokaa kama nguzo ambamo maumbo mengine yanajikita na kuitengeneza umbo kama la nyumba. Wazo lililoko nyuma ya mwonekano huu, ni kwamba UEM ni kama nyumba ya wanachama wote wa UEM, ambamo makundi yote ya udugu yanapumzika ndani yake.
- Mpangilio wa maumbo yaliyomo kwenye nembo hii, na nguzo zake vyote vinatengeneza alama ya msalaba, kuonyesha kwamba udugu na ufadhili umejengwa kwenye msingi wa mafundisho ya kikristo.
- Tuzo imetengenezwa kwa glasi (acrylic). Vifaa vya glasi vinawakilisha uwazi katika mambo yote ndani ya UEM

# V. Mifano halisi kutoka maeneo mbalimbali

## Kichwa: Diakonia · Maendeleo

### Ubunifu katika Udugu: Taasisi ya Eben-Ezer na Taasisi ya Alpha Omega katika kushirikisha makundi mengine ya udugu

Udugu kati ya taasisi ya Eben-Ezer ya kanisa la Lippe la mjini Lemgo, Ujerumani na taasisi ya Alpha Omega ya kanisa la ki-protestanti Karo Batak (GBKP) la mjini Kabanjahe Indonesia msingi wake ni mahusiano binafsi kati ya taasisi husika. Taasisi zote mbili zinatoa huduma za diakonia. Taasisi hizi zinahudumia watu wenyewe mahitaji maalum.

Taasisi ya Eben-Ezer inatunza na kuhudumia watoto, vijana na wazee wanaokadiriwa kufikia jumla ya watu elfu moja amba wote wanamatatizo ya utindio wa ubongo. Zaidi ya watumishi au wafanyakazi elfu moja wanawahudumia watoto, vijana na wazee hawa wanatunzwa na taasisi hii. Walengwa hawa wanajifunza kazi mbalimbali za mikono kama vile ufundi wa kutengeze vitu mbalimbali vinavyotokana na mbaa na miti, kuunganisha vitu mbalimbali vya umeme na vi-faa toka viwandani, kilimo na mambo madogo madogo



yanayohusu uchumi. Vijana wanaohuduria na kusoma kwenye shule ya Topehlen, wanapatiwa mahitaji yao muhimu na pia msaada wa kuelekezwa katika masomo yao.

Shule ya bweni inayomilikiwa na taasisi ya Alpha Omega (Alpha Omega boarding school), ni shule ya watu wenyewe mahitaji maalum pia. Inamabweni, mashamba, na nyumba. Shule hii inahudumia watoto, vijana na wazee amba jumla yao ni watu 86. Taasisi hizi mbili zimekuwa na udugu wa zaidi ya miaka 20 sasa. Udugu kati yao unaonekana kupitia njia mbalimbali kama vile kubadilisha uzoefu na kushirikishana juu ya kila upande unavyoendesha shughuli zake mbalimbali. Ufadhi-li katika miradi inachukua nafasi ndogo sana katika udugu baina ya taasisi hizi mbili.

"Tunajisikia furaha sana kuwa na urafiki na taasisi ya Eben-Ezer kwani kupitia urafiki huu tunapokea si mis-

aada tu, bali hata uzoefu wa namna ya kuendesha taasisi za namna hii na pia tunapata baraka za aina mbalimbali katika kufanya kazi na watu wenyewe mahitaji maalum", hayo yameandikwa na mchungaji Mestika Ginting kwenye barua yake ya Krismass ya mwaka 2014 kwenda kwenye taasisi ya Alpha Omega kule Lemgo. Mkurugenzi wa taasisi ya Alpha Omega aliitem-belea taasisi ya Eben-Ezer mwezi juni mwaka 2014 kwa majuma manne kwa minajili ya kufanya mazoezi ya vitendo (internship) na kujiona maeneo mbalimbali ya huduma zinazotolewa na taasisi hii. Taasisi ya Eben-Ezer Foundation ilikwishautangazia umma wa Indonesia kupitia vyombo vya habari juu ya ziara ya mkurugenzi kutoka Ujerumani, jambo ambalo lilivuta watu wengi sana. Jambo lililokuwa la kipekee kwenye mku-tano ule ni kwamba Taasisi ya Eben-Ezer, ilizialika si tu taasisi inazoshirikiana nazo kama vile taasisi ya Alpha Omega, bali iliwalialika pia viongozi wakuu wa taasisi zingine tatu zinazota huduma za diakonia kutoka kas-kazini ya Sumatra ambazo haziko kwenye kundi la udugu na taasisi ya Eben-Ezer. Taasisi hizo ni: Taasisi ya Hepata ya kanisa la kiprotestanti la Toba Batak (HKBP) inayohudumia watu wenyewe mahitaji maalum, Shule ya vipofu Yapentra ya kanisa la kiprotestanti la Indonesia (GKPI) na shule ya chekechea iitwayo Hannah Blindow ya kanisa la kiprotestanti la Nias (BNKP). Taasisi hizi zote zilikubali mwaliko kutoka Lemgo na hiyo ikawa fursa kwao ya kuona na kujifunza namna taasisi zinavyojishughulisha na huduma za diakonia nchini Ujerumani. Moja ya faida au matokeo ya ziara hii, ni kwamba taasisi hizi ambazo kabla ya hapo hazikushirikiana katika huduma wala kuwa wadugu, mara baada ya ziara hii wakaungana na kuanza wafanyakazi zao na kutoa huduma kwa ushirikiano wa kidugu mara baada ya kurudi nchini mwao Indonesia.

Mwaka mmoja baada ya ziara ya taasisi hizi nne ya kuitembelea Lemgo, ikasikika ndani ya UEM kwamba taasisi ya Eben-Ezer immealikwa kaskazini mwa Sumatra kuwa mwenyeji wa mafunzo kwaajili ya taasisi zote nne za diakonia ili kwamba kwa njia hiyo wafanyakazi wengine waweze kufaidika au kushirikishwa ujuzi ambaa viongozi hawa wa taasisi hizi nne walijifunza wali-pokuwa ziarani Lemgo Ujerumani. Kwasasa, watumishi wawili wa taasisi ya Eben-Ezer wanafanya mipango ya kuanda na kuendesha semina ya siku tano kwa viongozi na wafanyakazi wa taasisi zifuatizo: Alpha Omega, Hepata, na Yapentra kwa mwezi Januari mwaka 2017. Semina hii itajikita katika kufundisha namna ya kuwendesha watu wenyewe matatizo ya kushindwa kuelewa mazingira na watu na hivyo kukosa uwezo wa kukua

kiakili iwapasavyo (autism), kuhudumia watu wenye matatizo ya kuchangamka kusikokuwa kwa kawaida au kuchangamka kupita kiasi (hyperactivity), kuhudumia watu wenye mahitaji maalum binafsi, vifaa au vielelezo vinavyosaidia katika kuongeza uwezo wa mhusika kuelewa anapofundishwa (visual aid) na vifaa vya kufundishia. Wakati semina ikiendelea, ujumbe kutoka Lemgo nao utakuwepo ili kupata nafasi ya kufahamina zaidi na taasisi zote zilizotajwa hapo juu.

Taasisi ya Alpha Omega na taasisi ya Eben-Ezer kwa pamoja, zimefungua njia kwa taasisi zingine kuingia katika udugu huo ulioanzishwa miaka 20 iliyopita, hivyo kupanua wigo wa kushirikishana na kusaidiana kwa njia mbalimbali za namna ya kuendesha taasisi zao kwa ufanisi. Ushirikiano huu ni aina mojawapo ya mradi wa ubunifu kwani umeweza kufungua milango kwaajili ya kundi la tatu nje ya makundi au taasisi hizi mbili zilizoanzisha udugu.

Wazo la kuwa na semina iliyopangwa kufanyika mwaka 2017, ni wazo la taasisi za kidiakonia za Indonesia ambazo kwa pamoja zimefanya tathmini ya mahitaji walijonayo kama taasisi na kuona njia mwafaka nay a pekee ya kuyatua ni kwa njia ya semina ya pamoja. Upangaji na utekelezaji wa mradi vimejadiliwa kwa pamoja na makundi ya udugu, huku mjadala ukijikita katika mahitaji walijonayo wafanyakazi wa taasisi za

diakonia kaskazini mwa Sumatra na uwezo wa taasisi ya Eben-Ezer.

## Kichwa: Utetezi · Maendeleo · Uinjilisti

### Upandaji wa Miti Tanzania

IKaskazini magharibi mwa Tanzania, mpakani mwa Tanzania na nchi za Rwanda na Uganda, kuna ardhi tambarare lakini kwenye mwinuko wa karibia meta elfu moja kutoka usawa wa bahari. Eneo hili linaitwa Kituntu. Watu wa eneo hili ni maskini; asilimia arabolaini ya watu wa eneo hili ni maskini wa kupindukia. Kuanzia miaka ya 1990 watu hawa wa Kituntu wamekabiliwa na changamoto zinazosababishwa na mabadi-liko ya tabianchi. Rasillimali zao zimekuwa zikiharibika kwa kiwango kikubwa. Miti, vyanzo vya maji, na maliyasi nyininge vimekuwa adimu kila mwaka. Kwasa-babu hii, elimu juu ya mazingira ni hitaji kubwa na la lazima kwa watu wa Kituntu. Miti inahitajika kupanda tena ili kupunguza mmommonyoko wa udongo.

Haya ndiyo malengo ya KAKAUMAKI neno ambalo kirefu chake ni *Kampeni Kabambe Ya Utunzaji wa Mazingira Kituntu*. Mradi wa mazingira na upandaji miti wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania, Dayosisi ya Karagwe. Tangia zamani, malengo na mambo yote ya-husuyo mazingira kwa ujumla ni mambo ya kiroho na



yanaunganishwa na maisha ya uchaji na ibada. Kwa mfano, kwaya za sharika mbalimbali zimetunga nyimbo zinazohusu utunzaji wa mazingira, zikimtukuza Mungu kama muumbaji na huku zikitoa wito kwa watu kutunza mazingira. Nyimbo hizi zinaimbwa ibadani na kwenye mikutano ya uinjilisti. Hatua zingine zilizofikiwa hivi karibuni ni kwa kundi la vijana kujiunga pamoja na kusheherekeea kitu wanachokiita siku ya kuchukua hatua kwaajili ya mazingira (Youth Climate Action Day). Hii hufanya kila jumapili ya kwanza ya mwezi wa kumi na mbili.

Meneja wa kusimamia mradi aliajiriwa huku akisaidiwa na wainjilisti watatu. Wadau wengine 53 (waliojihuisha moja kwa moja na mradi) wakashirikishwa katika maandalizi ya upandaji wa miti. Usimamizi na ufuatiliaji wa mradi kwa hatua hizi za mwanzo ulifanyika kwa njia ya semina na kwa kulitembelea eneo la mradi mara kwa mara na kusomeana taarifa za mradi mara kwa mara.

Kwa miaka ya 2010 na 2011 pekee, miti 17,500 ilipandwa Kituntu ambapo kati ya miti hiyo yote ni miti 14,800 imeweza kuota vizuri. Wakati huo huo maamuzi ya dhati yalifikiwa ya kupanda miti mingine kwenye eneo la mteremko wa mlima sehemu ambayo ilikuwa im-eathiriwa sana na mmomonyoko wa udongo, lakini pia eneo hili halishindaniwi na watu kwaajili ya kilimo kwani siyo eneo rafiki kwa kilimo cha kawaida.

Moja ya faida kubwa ya mradi huu, ambao hapo kwanza ulipangwa kudumu kwa miaka miwili tu, ni kwamba watu binafsi pamoja na taasisi mbalimbali karibia jumla watu miatatu walioshiriki katika kutekeleza mradi huu, kipato chao kimeongezeka.

KAKAUMAKI imechangia sana katika ukuzaji na uen-ezaji wa elimu juu ya mazingira na utunzaji wa rasimali katika jimbo zima la Kituntu. Zaidi ya yote, mradi huu unahamasisha watu kufanya jitihada katika kuzuia mmomonyoko wa udongo na kuonyesha kwa wazi faida za upandaji miti. Njia za kitaalam zilizotumika katika kuandaa na katika kupanda miti pamoja na madhaiju tuliyojifunza kutoka kwenye miradi iliyopita, vimekuwa msaada katika kuhanakisha mradi huu una-fanikiwa na kuwa na faida kwa jamii. Pendekeso la mradi lilitanguliwa kwanza na upembuzi yakinifu wa hali ya mazingira na changamoto zote zinazoikibili jamii husika. Uandaaji wa mpango wa mradi ulichukua muda mrefu kukamilika, lakini hata hivyo mwisho im-eonyesha mpango huo ulistahili kufanyika kwa umakini kama ilivyofanyika. Hatua ya kwanza ilikuwa kuitisha semina na mikutano na ni kwa njia hii ya mikutano na semina, jamii ilishirikishwa wazo la kuwa na mradi huu. Wanajamii kwa ujumla walitumia uzoefu wao katika kutoa mchango wao wa mawazo kuhusiana na mradi pendekewa. Jambo lingine lililochangia ufanisi wa mradi ni uwepo wa hali ya kuaminiana na kushirikiana kwa dhati baina ya wasimamizi wakuu wa mradi, yaani mkuu wa jimbo husika, meneja wa mradi,

mchungaji wa eneo husika, wainjilisti, mtaalam mmoja wa kilimo na uchumi kutoka ofisi kuu ya kanisa kitengo cha maendeleo ya huduma za kanisa, na watu wa jamii ya Kituntu ambao walishiriki kwa moyo wote katika kuhanakisha mradi unafanikiwa.

## Kichwa: Uinjilisti

### **Kwaya ya kimataifa yenye waimbaji vijana kutoka Ujeruman, Kameruni na Tanzania**

"Tulia mahali ambapo nyimbo zinaimbwa, kwani wauvou hawana nyimbo." Sentensi hii ilisemwa na mtunzi na mwandishi mashuhuri wa mashairi Johann Gottfried Seume. Muziki au uimbaji wakati wote ni kama daraja linalowaunganisha watu wa tabaka na maeneo mbali mbali, lakini pia muziki ni lugha ambayo kila mtu anaielewa na inayowaleta pamoja watu wa tamaduni tofauti tofauti.

Mwanzilishi wa wazo la mradi wa kwaya ya umoja toka maeneo matatu wanachama wa UEM, liliasiwa na ndugu toka kundi la udugu la kanisa la kiinjili la Westfalia (EKvW). Ndugu huyu aliamua kuitumia dhana hii ya kuutumia muziki kama kiunganishi au kama chombo cha kuwaunganisha watu kutoka tabaka au maeneo tofauti tofauti.

Kwa muda mrefu usharika wa Soest umekuwa katika uhusiano wa udugu na usharika wa Grand Nord wa kanisa la kiinjili la Kameruni (EEC). Wakati huo huo usharika wa Arnsberg umekuwa kwenye uhusiano wa udugu na usharika wa Ihembe wa kanisa la kiinjili la kilutheri Tanzania, dayosisi ya Karagwe (ELCT-KAD). Hivyo mradi wa kwaya hii ya kimataifa ni jitihada za kujaribisha aina nyingine mpya ya ushirikiano wa kiudugu, tofauti na mfumo wa ushirikiano uliozoeleka wa viongozi wa udugu kutembeleana. Kupitia mradi huu, waimbaji vijana walipata nafasi ya kukutana na vijana wengine wa kikristo kutoka tamaduni mbali mbali, wakafundishana nyimbo za tamaduni mbalimbali na kwa njia ya nyimbo zao wote kwa pamoja waliweza kubeba ushuhuda mmoja juu ya namna injili ya Yesu Kristo ilivyo na nguvu.

Katika kuandaa kwaya itakayozunguka kufanya matamasha sehemu mbali mbali za ujeruman, ilibidi kutanguliwe na maandalizi ya kundi dogo la kwaya nchini kameruni, Ujeruman na nchini Tanzania. Kila kwaya ilifanya mazoezi ya nyimbo zake kabla kwaya ya umoja hajakutana bado huko Westfalia Ujeruman. Baada ya waimbaji wote kukutana, kufahamiana na kugawana majukumu, waimbaji hawa wanaume kwa wanawake wakaanza huduma ya uimbaji kwa kuzunguka na kuimba katika sharika na kwenye mashule mbali mbali.

Changamoto ya kwanza ambayo waimbaji wote walipaswa kukabiliana nayo ilikuwa ni utofauti wa lugha.

Pamoja na kwamba kujua kuzungumza kingereza ili-kuwa sifa mama kwa waimbaji waliotakiwa kuunda kwaya ya umoja, bado baadhi ya waimbaji walikuwa wakizungumza kiingereza kwa shida. Utata mwininge ulijitokeza pale ilipogundulika kuwa haikuwa rahisi kuwapata vijana wa kijerumanii ambaa wangelikuwa tayari na pia kuwa na muda wa kutosha kuwasaidia waimbaji hawa wageni katika mambo mbali mbali kuanzia mwanzo hadi mwisho wa kukaa kwao Ujerumanii.

Kuanzia mradi ulipoanza, waandaaji wamefanya tathmini ya mradi huu wa kwaya kwa kina na kuorodhesha mambo yote yaliyofitokeza ili kuweza kuwapatia naka-la makundi yote ya udugu yanayopenda kusoma tath-

mini hii. Muhtasari wa tathmini kutoka kwa waandaaji wa mradi ni huu: Uwepo wa kwaya ya mradi na matamasha yote yaliyofanywa na kwaya kwenye mae-neo ya sharika za Soest na Arnsberg, kulifanya kazi au huduma za udugu za sharika hizi mbili kujulikana zaidi kwa jamii. Matamasha yaliyofanywa na vijana hawa yalikuwa ni uthibitisho tosha kwamba mradi umeweza kutumia vema utajiri wa tamaduni za makanisa mbali mbali ya udugu, ambazo mradi umeweza kuziungani-sha na kuzitumia katika kudumisha udugu.

Mradi huu uliotekelawa kwa majuma matatu, uli-fadhiliwa kwa michango kutoka sharika mbalimbali, sadaka, fedha kutoka wafadhili mbali mbali na fungu la fedha lililotolewa na UEM



# VI. Vielelezo

## a) Mfano wa Makubaliano juu ya Mradi

Maelezo juu ya Mradi

Jina la Mradi

Washirika wa mradi (Nani unategemea kufanyanao mradi)  
na wanaotoa maamuzi pamoja na anwani zao

Kuna wafanyakazi wangapi na wale wa kujitolea  
wangapi watafanya kazi kwenye mradi?

Muda wa utekelezaji wa mradi

Jumla ya fedha zinazohitajika kwa ufadhilli wa mradi

Mchango kutoka kwa aliyesababisha kuwepo  
kwa mradi (mwanzilishi wa mradi)

**Kuuelezea Mradi wenye**

**Walengwa**

Maelezo juu ya namna jamii inavyojisikia kuhusika au kuguswa na mradi husika, kazi za wenyeji au shughuli za  
wenyeji wa mahali mradi utakapotekelezwa, uwiano wa idadi katika wanaume na wanawake, je kundi la  
walengwa wamehusishwa na kuwezeshwa kutoa maoni yao juu ya mradi kuanzia hatua za mwanzo za upangaji  
wa mradi husika? Kwa namna gani au kwa njia gani walengwa waliweza kutoa maoni yao?

**Mahali / Eneo Mradi utatekelezwa**

Ni eneo gani ambapo mradi utatekelezwa? Maelezo juu ya miundombinu ya kiuchumi na kijamii, miundombinu,  
hali ya hewa na mazingira

**Hali ya mwanzo kabla ya mradi/ Maelezo juu ya matatizo au changamoto**

Orodhesha sababu zote zinazoonyesha kwamba mradi pendekezwa ni muhimu. Je kumewahi kutekelezwa mradi  
kama huo kwenye ukanda unaoombewa mradi na je kuna uzoefu wowote uliopatikana toka kwenye mradi  
uliopita? Je mradi pendekezwa umejumuishwa kwenye mipango ya kanisa, au umepata kibali cha kanisa? Je mradi  
huu umezingatia mambo muhimu na kuyatilia maanani, kama vile uchumi, mazingira, jamii husika, utamaduni wa  
watu wa eneo husika, dini za watu wa eneo husika?

**Hatua zilizopangwa kuchukuliwa**

Nini hasa kimepangwa kufanyika? Nani anawajibu gani, na ni vigezo gani vimetumika katika kugawana wajibu?  
Nini mchango kutoka kwa waliopendekeza ufadhilli wa mradi (mchango wa kifedha, mchango wa ujuzi au  
nguvukazi, michango isiyo ya kifedha)

### Malengo ya Mradi

Ni malengo gani ambayo yanategemewa kufikiwa mradi utakapokuwa umefikia ukomo? Ni malengo gani ya mpito yanayotegemewa kufikiwa? Eleza ni muhimili gani wa UEM kati ya mihimili mitano ambayo itakuwa ndiyo dira katika upangaji wa mradi?

### Mpango wa Namna ya Kupeana Taarifa

Nani atakuwa anatoa taarifa, lini, taarifa gani, kwa nani?

### Usimamizi/Ukaguzi

Je ni mpango upi utatumika katika usimamizi au ukaguzi wa mradi? Nani anaongoza mradi? Kwa makongamano au warsha na matukio yanayofanana na hayo, hakikisha unatoa taarifa ya kina inayotaja hata idadi ya watu waliohudhuria, mbinu za uweshehaji zilizotumika, utaratibu (programu) na wataalam walioalikwa kama wawezeshaji. Kwa miradi ya ujenzi, tafadhali mpangokazi wa ujenzi, pamoja na hatua mbali mbali za utekelezaji wa ujenzi lazima viunganishwe kwenye taarifa. Je ukaguzi wa mahesabu umeunganishwa kwenye taarifa?

### Mradi Endelevu

Je wadugu waliomo kwenye nchi inayopewa ufadhili wa mradi, wanao uwezo wa kuupokea mradi husika pale wanapohitajika kufanya hivyo na je baada ya kuupokea wanauwezo wa kuufanya kuwa mradi endelevu hata baada ya muda uliokuwa umekusudiwa kwa mradi huo kufikia ukomo? Je rasilimali zinazohitajika kwa mradi zinaweza kununuliwa kwenye soko la ndani? Je kuna watu au mashirika yanayoweza kutunza uaminifu hasa pale yatakapohitajika kuleta vipuri vinavyohitajika katika mradi pale vile vya awali vikiharibika au kuchakaa? Je rasilimali zinazotakiwa kutumika kwenye mradi zinakubalika na jamii husika na je matumizi hayo hayatachangia katika kuharibu mazingira?

### Hatari zinazoweza kutokea wakati wa utekelezaji wa mradi

Ni hatari zipi zinaweza kusababishwa na mradi au kutokea wakati wa kipindi cha kuendesha au kutekeleza mradi husika? Kipi kifanyike ikiwa mipango iliyopangwa ya kukabiliana na hatari hizo hautaleta ufanisi au itashindwa kudhibiti hatari hizo?

### Tathmini

Je kuna mipango yoyote iliyokwishakupangwa tayari kuhusiana na tathmini itakayofanywa na wataalam wa ndani/ au wataalam wa nje?

### Gharama zote na Ufadhilli

**Matumizi** (uvekezaji, gharama za uendeshaji, gharama za malipo kwa watumishi/wafanyakazi)

**Mapato** (juhudhi za aliyesababisha mradi kuanzishwa, ruzuku zingine: je vyanzo gani vingine vya fedha ambavyo vipo kwaajili ya kusaidia mradi? Je mradi huu utapelekwa pia kwa makundi mengine ya udugu ili kupatiwa ufadhilli?)

Mahali, Tarehe

Sahihi za wadugu au makundi yote ya udugu yanayohusika na mradi

## b) Maombi ya Kibali cha UEM cha mradi

### Mradi na maelezo

Jina la mradi

Washirika katika mradi wa udugu na wafanyamaamuzi wote na anwani zao

26

Muda wa mradi

Maelezo mafupi (yenye kutosheleza) juu ya mradi

### Vigezo

#### 1. Umoja katika maazimio

Je maazimio juu ya mradi huu, yalifikiwa na pande zote zinazohusika na mradi husika?

#### 2. Umoja au ushirika katika kupanga na kuendesha miradi

Ni kwa namna gani mradi ulipangwa, ukasimamiwa, na ukafanyiwa tathmini kwa umoja au ushirika? Ni kwa kiwango gani mradi ulifadhiliwa kwa ushirika baina ya wafadhilli na washiriki wote wa mradi kwa njia ya fedha na kwa njia ya kuchangia vitu vingine mbali ya fedha?

#### 3. Mtazamo tofauti tofauti katika kupanga

Ni mhimili upi katika mihimili mitano ya UEM uliotiliwa maanani wakati wa kupanga na wakati wa utekelezaji wa mradi? Tafadhali elezea Zaidi.

#### 4. Msaada wa elimu

Ni hatua gani za uelimishaji zilizochukuliwa au kufikiwa? (semina, kampeni mbalimbali, n.k.) Hatua zitafutana na pamoja na mradi.

#### 5. Huduma za Uhusiano wa Umma

Ni huduma zipi za uhusiano wa umma zimejitekeza (mfano, rufaa mbalimbali na taarifa ibadani, jarida za sharika mbalimbali, tovuti, vyombo vya habari). Tafadhali toa mifano.

Mahali, Tarehe

Sahihi za wahusika wote walioshiriki toka makundi ya udugu

# Uchapishaji

Mchapishaji:

United Evangelical Mission (UEM)  
Rudolfstrasse 137, 42285 Wuppertal, Germany  
[www.vemission.org](http://www.vemission.org)

Mhariri Mkuu:  
Brunhild von Local

Waandishi: Uli Baege, Frauke Bürgers,  
Kristina Neubauer, Jörg Stähler

Picha/michoro: Britta Kläffgen

Muundo na Mpangilio: MediaCompany –  
Agentur für Kommunikation GmbH

Kufanyika kwa upya: Desemba 2015

## Anwani

### Afrika

Ofisi ya Ukanda wa Afrika – Dar es Salaam  
Luther House, ghorofa ya pili, Sokoine Drive  
P.O.Box 75240  
Dar es Salaam, Tanzania  
✉ [africaregional@vemission.org](mailto:africaregional@vemission.org)

### Asia

Ofisi ya Ukanda wa Asia - Medan  
Jl. Selamat Ketaren No. 100 Pancing  
Medan Estate 20371  
Sumatera Utara, Indonesia  
✉ [uem.medanoffice@gmail.com](mailto:uem.medanoffice@gmail.com)

### Ujerumani

Udugu ndani ya UEM – Wuppertal  
Rudolfstrasse 137  
42285 Wuppertal, Germany  
✉ [partnerships@vemission.org](mailto:partnerships@vemission.org)



